MAELEKEZO YA ELIMU KWA MCHIMBA MADINI

Maelekezo kuhusu haki na wajibu, kulipa kodi, mihungano ya ushirika, usalama katika kazi, na mashurti ya CIRGL na OCDE

1. Haki na wajibu wa wachimba madini



Somo ya 1: *Inakatazwa kwa wachimba madini wa mikono kufanya kazi zao katika maneo ya mashirika (concession minière) za uchimbaji madini bila ruhusa ya mwenyeji (concessionnaire)*

Somo ya 2 : *Mihungano ya ushirika ya wachimbaji (coopératives) zinapashwa kulinda eneo zao za uchimbaji (sites miniers validés) zao ili watu wasioruhisiwa na sheria wasishiriki uchimbaji madini, piya na kuepuka kuchanga madini yao na ya eneo zisizokubaliwa (site non validés).*



Somo ya 3 : *Wachimba madini wanapashwa tunza mazingira karibu na kazi ya _ inakatazwa kukata miti kiolela pembeni na kazi yao*

2. Kodi za kulipa katika sekta ya madini



Somo ya 4 : *Wachimba madini wanapashwa pinga (katala) kulipa kodi (mlipo) isiyokuwa na msingi kiserekali (paiement non prévu par la loi).*

Somo ya 5 : *Wachimba madini wanapashwa katala kulipa kodi ao malipo juu yakubeba ao kubebesha madini katika eneo moja (transport intersites des minerais : toka eneo yakuchimba kuelekeya eneo yakusukuliya).*

Somo ya 6: *Wachimba madini wanapashwa lazimisha kupewa kidhibitisho kwa kila malipo wanayofanya*



Somo ya 7 : *Wachimba madini wana shurti (obligation, devoir) yakulipa kodi za serekali kwa idara usika.*

3. Mihungano ya ushirika ya wachimba madini

Somo ya 8 : *Muhungano wa ushirika sio shirika chakuja kushurutisha ao kunyanyasa wachimba madini. Inapashwa kuwashirika yakutatuwa shida ao matatizo yao*



Somo ya 9 : *Uhundwaji wa Muhungano wa ushirika inapashwa hanza na changizo ya mawazo toka wanamemba waazilishi. Nayo inapashwa leta jibu kwa haja na shida za wanamemba wake.*

4. Usalama wa kazi katika madini

Somo 10 : *Shimo zinapashwa kutengenezwa kwa kukulinda usalama wa wachimba madini.*

Somo ya 11: *Utumiyaji wa kapata ndani ya migodi, inaregeza mwamba na kupunguza usalama ndani ya mgodi. Piya inapigwa marufuko na sheria ya inchi kutumiya kapata katika migodi*



Somo ya 12: *Inaoba kila mchimba madini awa na vifaa vya kujilindiya usalama (godio "kiato nzuri ya kazi", casque, cache-nez, bouche-oreille, gans, lunette (miwani), salopette, ...)*

SOmo ya 13: *Utumiyaji wa kemikali inapaigwa marufuko na sheria. Utumiyaji wake unasababisha magondjwa mengi ikewemo magondjwa ya Kansa*

Somo ya 14: *Mgodi unapashwa kujengwa ao kukarabatiwa vizuri, ukiwa na vifaa vya kuingiza mwangaza – hewa – na kutowa maji kwa kila wakati ili kupunguza ajali za kazi. Mwangaza inapashwatolewa na taa zisizotiya kifukuto ndani ya mgodi (lampe à cathode froide) kwa kukinga ukosefu wa*

5. Shuri ya cheti ya madini

Somo ya 15: *Sheria inakataza wanawake wajawazito na watoto kufanya kazi za madini. Kupatikana kwao ndani ya eneo fulani hupelekeya kuwekwa kwa alama nyekundu kwa eneo hiyo.*

Somo ya 16: *Sheria inakataza wachimba madini kulipa kodi ao malipo yoyote kwa wajeshi (ikiwemo kuwapa madini ao kuwapa saa za kuchimba mu mugodi). Kila ukengeukaji waw a sheria hiyo inafanya eneo ao site iwe nyekundu. Piya inakatazwa kwa wajeshi kutiya barrière ao kuingiya mu eneo ya wachimba madini.*

Somo ya 17: *Eneo inayomilikiwa na kikundi chenye kumiliki silaa (groupe armé) ina alama nyekundu. Madini za eno ya namna iyo hazirusiwi kwa uchuhuzi*

Somo ya 18 : *Wanawake wana haki yakutumika kazi za madini, ikiwa sio wajawazito. Wana haki ya kuwa wanamemba wa mihungano ya ushirika ya wachimba madini*



Somo ya 19 : *Inapigwa marufuko kuchanga madini ya eneo yenye kukubaliko (site validé vert) na ya eneo isiyokubaliwa kwa kazi za madini (site rouge). Penginepo, madini yote inakuwa nyekundu.*

6. Watu wanaokataliwa ku kazi za madini mu DRC

Somo ya 20 : *Wafanya kazi wa Idara ya madini, wa SAESSCAM, wa ANR, Jeshi, polisi, wafanyakazi wa mahakama, Msimamizi wa Bwami ao sekta (chefferie ao secteur), kiongozi wa tarafa na kila anayetumika katika makazi za serekali harusiwiya kuwa na : mugodi, Concasseur, loutra, motopompe, maison d'achat des minerais. Wanakatazwa piya kuhuza ao kuwa na ma saa za kuchimbisha dani ya shimo.*

*Imeandaliwa na **Max Impact** asbl kwa msaada wa **UE** kupitiya shirika la **GIZ***